



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA CHEMBA
Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji.



FAX/ SIMU 026 2360175
E - MAIL: ded@chembadc.go.tz

01/10/2024

TANGAZO KWA UMMA

**DIRISHA LA UTOAJI MIKOPO KWA VIKUNDI VYA
WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU
LIMEFUNGULIWA RASMI 01/10/2024 NAKUENDELEA**

**(Limetolewa kwa kuzingatia Sura ya 290 kifungu cha 37A (4)
ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa)**

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA, ANATANGAZA UWEPO WA FEDHA KWA AJILI YA KUKOPESHA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU KWA MWAKA WA FEDHA **2024/2025**. VIKUNDI VYENYE SIFA VINATAKIWA VIJISAJILI NA KUOMBA MKOPO KUPITIA OFISI ZA WATENDAJI WA VIJJI ZILIZOPO KATIKA MAENEO YA VIJJI.

VIKUNDI VINAPASWA KUWA NA SIFA ZIFUATAZO KABLA YA KUOMBA MKOPO: -

- 1. Wanakikundi wawe ni raia wa Tanzania wenye akili timamu na umri wa miaka 18 na kuendelea isipokuwa kwa kundi la vijana ni miaka 18 hadi 45.**
- 2. Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenye Ulemavu lazima kiwe kimetambuliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Mfumo wa kieletroniki wa utoaji na Usimamizi wa mikopo.**
- 3. Kikundi kiwe kinajishughulisha na ujasiriamali au kinakusudia kuanzisha shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati;**
- 4. Kikundi cha Wanawake na Vijana lazima kiwe na wanachama kuanzia watano (5) na kuendelea, wakati**

kikundi cha watu Wenye Ulemavu kinatakiwa kuwa na wanachama wasiopungua wawili (2) isipokuwa pale ambapo Menejimenti ya Halmashauri imejiridhisha kuwa mlemavu amekosa mtu mwingine wa kushirikiana naye katika mradi kusudiwa anaweza kuwa mmoja (1), hii ni kwa mujibu wa kanuni ya 6(1);

- 5. Kikundi kiwe na akaunti benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi na yenye akiba**
- 6. Kikundi kisiwe na deni la Mkopo wa Halmashauri au Taasisi yoyote ya kifedha.**
- 7. Kikundi kisiwe na wajumbe wenye ajira rasmi.**

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA MKURUGENZI
MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA**

**“Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi Jitokeze kushiriki
Uchaguzi”**